

UKWELI UNAPASWA KUJUA.

DOZI ZA KUIMARISHA KINGA YA MWILI

Chanjo za COVID-19 ni faafu.

Chanjo za COVID-19 hukulinda dhidi ya ugonjwa mbaya, kulazwa hospitalini, na kifo. Kupata chanjo zote za COVID-19, ikiwa ni pamoja na kupata dozi za nyongeza unapostahiki, ni muhimu ili uwe na ulinzi zaidi.



DOZI ZA KUIMARISHA KINGA YA MWILI NI SALAMA

Dozi za kuimarisha kinga ya mwili dhidi ya COVID-19 ni sawa na chanjo halisi, ambazo zimethibitishwa kuwa salama kwa mamia ya mamilioni ya watu. Ni kawaida kupata madhara madogo. Ni nadra sana kupata madhara makubwa.



DOZI ZA KUIMARISHA KINGA YA MWILI HUKUSAIDIA KUWA SALAMA

Dozi za kuimarisha kinga ya mwili hukulinda kikamilifu dhidi ya kuambukizwa COVID-19.



Sindano za kuongeza nguvu ni kawaida kwa chanjo nyingi. Kwa mfano, chanjo za pepopunda zinahitaji dozi za kuimarisha kinga ya mwili kila baada ya miaka 10 kwa watu wazima.

Wanasayansi wamegundua kwamba nguvu za baadhi ya chanjo katika kumkinga mtu hupungua baada ya muda fulani, na dozi za kuimarisha kinga ya mwili huwasaidia kuwa salama. Dozi za kuimarisha kinga ya mwili dhidi ya COVID-19 hufanya kazi kwa njia sawa.



Nani anaweza kupata dozi ya kuimarisha kinga ya mwili

Dozi za kuimarisha kinga ya mwili huwapa watu wote ulinzi zaidi, lakini ni muhimu haswa kwa watu walio na matatizo ya kiafya, au wale ambao kazi au hali ya maisha inawaweka katika hatari kubwa ya kuambukizwa COVID-19 au kuwa wagonjwa sana.

Dozi za kuimarisha kinga ya mwili zinatolewa bila malipo kwa watu wote bila kujali hali yako ya uhamiaji, au ikiwa una bima ya afya au kitambulisho.



PATA ULINZI ZAIDI

Njia bora ya kulinda familia yako, jumuiya yako na kujilinda mwenyewe dhidi ya COVID-19 ni kupokea chanjo ipasavyo. Kupata chanjo zote kunamaanisha kupata dozi zote mbili za chanjo inayodungwa mara mbili, na kisha kupata dozi zozote za nyongeza unazostahiki.

Endelea kuvaa barakoa, kutokaribiana na watu, na kukaa nyumbani ukiwa mgonjwa, ili uwalinde watu wote.

**JILINDE. LINDA JAMII YAKO.
PATA CHANJO.**